

# OPENER STD 6 TERM 2 2020

## KISWAHILI

NAME.....

Learner's Number

Gender Boy

Girl

County name ..... County code

Sub county name ..... Sub county code

School name ..... School code

The grid below is to be filled by the teacher after marking the learner's work

|                      | Level 1 | Level 2 | Level 3 | Level 4 |
|----------------------|---------|---------|---------|---------|
| Numbers<br>1-15      |         |         |         |         |
| Measurement<br>16-23 |         |         |         |         |
| Geometry<br>24-25    |         |         |         |         |

Soma vifungu vifuatavyo. Vina nafasi 1 mpaka 15. Kwa kila nafasi, umepewa majibu manne hapo. Jaza kila neno kwa kuchagua jawabu lifaalo zaidi.

Siku hiz, \_\_\_\_\_ waonyeshi 1 kwa wakubwa wao. Utamsikia mtoto 2 na mzazi kama kwamba ni wa 3 lake. Wengine hata 4 matusi wakubwa wao. Hapo 5, matukio ya aina hii 6 kama 7. Watoto waliwaheshimu wazazi na hata ndugu 8 wakubwa. Isitoshe, ubaguzi 9 katika malezi. Hata majirani 10 mtoto kwa hali na mali.

1. A. adhabu                      B. adabu                      C. tabia                      D. vitendo
2. A. akijibu                      B. akijibiwa                      C. akijibizana                      D. akiwajibu
3. A. rika                      B. umri                      C. hirimu                      D. miaka
4. A. huwatemea                      B. huwarushia                      C. huwapa                      D. huwabwagia
5. A. samani                      B. majuzi                      C. zamani                      D. karibuni
6. A. iliadimika                      B. yaliadimika                      C. paliadimika                      D. ziliadimika
7. A. wali wa daku                      B. uta na upote                      C. tui na maziwa                      D. shilingi kwa ya pili
8. A. yao                      B. wao                      C. zenu                      D. zao
9. A. hawakuwepo                      B. haukuwepo                      C. haikuwepo                      D. hazikuwepo
10. A. waliwatuza                      B. walitua                      C. walimtunza                      D. walikutuza

Safari yetu ilikuwa 11 12 ilituchukua karibu muda wa 13 sita. Tulifika jijini mwendo wa saa sita 14. Tulikuwa na uchovu 15. Mama alimpigia ami simu akaja kutuchukua pale kituoni.

11. A. mrefu                      B. refu                      C. kurefu                      D. ndefu
12. A. ili                      B. kwani                      C. ndio                      D. bali
13. A. saa                      B. masaa                      C. lisaa                      D. malisaa
14. A. alasiri                      B. magharibi                      C. adhuhuri                      D. asubuhi
15. A. mwingi                      B. mingi                      C. nyingi                      D. mengi

Kuanzia nambari 16 mpaka 30, jibu kulingana na maagizo.

16. Chagua orodha ya viungo vya mapishi  
A. wali, biriani, dania  
B. pilipili hoho, viazi nyanya  
C. kitunguu, mdalasini, iliki  
D. ndimu, papai, wimbii

17. Andika wingi wa sentensi ifuatayo:

Shati alilionunulia ni zuri.

- A. Shati walizotununulia ni nzuri.
- B. Mashati waliyotununulia ni mazuri.
- C. Mashati waliyotununulia ni nzuri.
- D. Shati walizoninunulia ni wazuri.

18. Shairi lenye misharoro mitatu katika kila ubeti huitwa

- A. tathlitha                      B. tarbia
- C. takhimisa                      D. tashnia


19. Chagua methali inayotushauri turekebishe kasoro mapema.  
 A. Kidole kimoja hakivunji chawa.  
 B. Ajizi ni ufunguo wa umaskini.  
 C. Kikulacho ki nguoni mwako.  
 D. Usipoziba ufa utajenga ukuta.

20. Kamilisha:  
 Je, harusi hiyo ilikuwa na magari \_\_\_\_\_?  
 A. zipi B. ngapi  
 C. mangapi D. yangapi

21. Sehemu ya jicho inayoona huitwaje?  
 A. nyusi B. mboni  
 C. kope D. gololi

22. Neno lipi ni kivumishi cha pekee?  
 A. kingine B. wengi  
 C. wachafu D. gani

23. Tumia kiunganishi kifaacho kujazia pengo.  
 Mama alinishauri nisisivute sigara \_\_\_\_\_  
 kunywa pombe yoyote.  
 A. wala B. lakini  
 C. bali D. na

24. Maumbò   
 A. Pia, mistari, sulubu  
 B. Mche, mistatili  
 C. Kikombe, pembe tatu  
 D. Mche, mistari sambamba

25. Tegua kitendawili kifuatacho:  
 "Unda langu la ajabu, lina nyama nje na ngozi ndani."  
 A. Yai B. Firigisi  
 C. Tomoko D. Fenesi

26. Akisami  $\frac{3}{4}$  kwa maneno ni  
 A. robo tatu B. thuluthi  
 C. humusi tatu D. thuluthi mne

27. Tumia kirejeshi -ndi- kwa usahihi.  
 Wageni \_\_\_\_\_ wanaopumzika sebuleni.  
 A. ndinyi B. ndiyo  
 C. ndio D. ndiye

28. Kamilisha sentensi ifuatayo:  
 Mkimbaji huyo alikimbia \_\_\_\_\_ za a'abu.  
 A. kimbia B. kimbilio  
 C. ukimbaji D. mbio

29. Kanusha:  
 Mvua imenysha sana.  
 A. Mvua haikunyeshi sana.  
 B. Mvua hainyeshi sana.  
 C. Mvua haitanyeshi sana.  
 D. Mvua haijanyeshi sana.

30. Ukimkosea mtu bila kukusudia utamwambia  
 A. simile B. niwie radhi  
 C. pole D. asante

Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali 31 - 40

"Nendeni zenu **fukara** nyingi," alisema shauo huku akijitana kifuu kwa kiburi. Hapo alikuwa ameletewa shilingi elfu mbili na kakaye mkwasi kwelikweli. Muda huo alikuwa ametembelea na masahibu zake wawili waliomwomba atoe mchango wake kwa kijana aliyetakikana kusafiri ng'ambo kwa masomo.

"Tumeishi hapa na shauo katika ukata, leo kakaye anmfadhili ameanza kuwa **mkono birika**?" Alisema rafiki yake mmoja kwa mshangao.

Shauo hakutaka kufanya kazi yoyote. Tangu kakaye abarikiwe na Maulana kwa utajiri mkubwa, Shauo alipenda kukaa mchana kutwa sebuleni kwake akitazama runinga. Shida zake zote alizisukumia kakaye. Alikuwa mzembe kiasi cha kuwa hata kufyeka nyasi kwenye kiunga cha nyumba yake ilimhitaji kumtuma mkewe, "Mama Jada, hebu mtume binti akamwambaye ami yake kuwa nyasi zinahitaji kufyekwa. Atupe shilingi mia mbili tuajiri mtu kibarua". Alisema huku akenyoosha miguu yake.

Muda haukuwa mrefu mambo yakachukua mkondo tautauti. Kakaye Chigoto alitiwa mbaroni na askari. Kumbe alikuwa akifanya biashara ya dawa za kule ya! Mali yake yote aliyapata kwa njia ya magendo. Hakimu alitoa hukumu na pigo kubwa likaangukia, amii yake akiwemo kakaye. Mali yake yote yalitaifishwa na utajiri wake ukaporomoka kama mnara wa karata.

Shauo alibaki kuama kidole na kujishika tama usiku kucha. Maisha yalimbadilikia mithili ya rangi ya kinyonga. "Jamani ni fakula nini? Wanangu watalipiwa karo na nani? Nani ataninunulia nguo?" Alijiuliza maswali mengi yaliyokosa majibu. Maisha yake yalikuwa magumu. Alikula mwata. Alianza kujuta na kujiuliza sababu ya kutojitegemea lakini ilikuwa bure. "**Maji yakimwagika hayazoleki**" Alilia sana alipoona vile shida zilivyomwandama moja baada ya nyingine kwani fimbo aliyoitengea ilivunjika. Shauo alipata funzo kuwa ni vyema mtu kujitegemea kwani, "**Mtumai cha ndugu hufa maskini**".

- |  |  |
|--|--|
| <p>31. Neno <b>fukara</b> kama lilivyotumika halina maana sawa na,<br/>A. maskini                      B. mkata<br/>C. mchochole                  D. kapera</p> <p>32. Maisha ya Shauo yalimwendea vizuri kwa kuwa<br/>A. biashara zake zilimletea faida.<br/>B. mwanawe alianza kumpa msaada.<br/>C. marafiki zake walimletea shilingi elfu mbili.<br/>D. alianza kupewa msaada na nduguye.</p> <p>33. Wakazi walikuwa na ushirikiano kwa kuwa,<br/>A. walichanga ili kijana aende ng'ambo.<br/>B. walishangazwa na maringo ya Shauo.<br/>C. Walienda kuomba mchango wa Shauo<br/>D. Walitafuta msaada kwa kakaye Shauo</p> <p>34. Msemo <b>mkono birika</b> unarejelea mtu mwenye tabia ya,<br/>A. kiburi<br/>B. ukwasi<br/>C. uchoyo<br/>D. ukarimu</p> <p>35. Ni tabia gani hasa inayoonyesha uvivu wa Shauo?<br/>A. Kukaa sebuleni kutazima runinga.<br/>B. Kushindwa kufyeka nyasi kwenye kiunga.<br/>C. Kumtuma bintiye kwa ami yake.<br/>D. Kuwafurusha marafiki waliomtembelea.</p> | <p>36. Mambo yalichukua mkondo tofauti,<br/>A. Shauo aliposhikwa na polisi.<br/>B. Kakaye Shauo alipotiwa nguvuni.<br/>C. Kakaye alipokataa kumsaidia.<br/>D. Shauo alipokataa kutoa mshango.</p> <p>37. Biashara aliyofanya kakaye Shauo ilikuwa,<br/>A. haramu                      B. halali<br/>C. ngumu                      D. rahisi</p> <p>38. Nduguye Shauo alimfanyia haya yote isipokuwa,<br/>A. kumnunulia mavazi<br/>B. kumlipia kodi<br/>C. kumnunulia chakula<br/>D. kuwalipia wanawe karo.</p> <p>39. Methali '<b>maji yakishamwagika hayazoleki</b>' ina maana kuwa,<br/>A. ni vyema kushughulikia mambo yanapoanza kuharibika.<br/>B. mtu mvivu wakati wote huishia kusumbuka maishani.<br/>C. kutegemea misaada ya ndugu huleta majuto maishani.<br/>D. mambo mengine yakishaharibika ni vigumu kuyarekebisha.</p> <p>40. Kifungu hiki kinatufunza,<br/>A. tuwathamini ndugu zetu kuliko marafiki.<br/>B. ni vyema kushirikiana na wanajamii wengine.<br/>C. umuhimu wa kujitegemea maishani.<br/>D. matumizi ya dawa za kulevya ni hatari.</p> |
|--|--|

**Yasome makala haya kisha ujibu maswali kuanzia 41 mpaka 50**

Ufisadi ni uovu unaotendwa na watu bila kutaka matendo haya yajulikane na adinasi wengine. Jambo hili huangamiza maisha ya wananchi katika jamii na nchi. Ufisadi huhusisha matumizi mabaya ya mali ya umma, kupokea na kutoa rushwa na mienendo mingine **inavokiuka sheria**. Nchi nyingi hasa za Kiafrika zimefilisika kutokana na ufisadi ambapo watu wachache wanajitajirisha kupita kiasi huku maskini wakiendelea kuishi maisha ya ajabu.

Matumizi mabaya ya mali ya umma yamekithiri katika nchi nyingi. Tabia hii hutekelezwa mara nyingi na viongozi. Kiongozi anapopewa pesa za kusaidia eneo analoongoza, unampata akitumia pesa hizo kwa kujinunulia magari ya kifahari. Tabia hii inawaacha wananchi wakiangamia.

Kupokea na kutoa rushwa kumekuwa kama ibada miongoni mwa watu wengi wakiwemo polisi, mahakimu na wengine wengi. Tabia hii inawafanya watu wanaofaa kupata huduma fulani kuikosa huku wale wasiofaa kuipata wakiipata. Mahakimu wanawaachilia wahalifu warudi kwenye jamii badala ya kuwahukumu. Polisi nao wanawaacha madereva wasio na vidhibitimwendo kuendelea na safari zao. Haya yote ni kwa sababu ya hongo.

Ufisadi huambatana na madhara yake ambayo huja baada ya ufisadi wenyewe kutendeka. Kwa kweli, majuto ni mjukuu, wahenga hawakukosea. Baada ya wahakimu kuwaachilia wahalifu hawa hurudia uovu uo huo tena. Hiyo huwafanya wananchi waadilifu kuendelea kuteseka bure bilashi. Magari yasiyokuwa na vidhibitimwendo yanapokubaliwa kuendelea na safari, ajali hutokea na vifo vya watu wengi hutokea. Ufisadi kwa jumla huivuta nchi nyuma badala ya kuipeleka mbele.

Wananchi wote wanastahili kuyafahamu masuala yote yanayohusu ufisadi ili kujiepusha nayo na pia kushiriki katika kuipiga vita. Aidha, polisi pamoja na mahakimu wasiotekeleza wajibu wao kwa njia inayofaa wanafaa waachishwe kazi. Mafisadi hawa wakiadhibiwa watakoma tabia zao na pia litakuwa funzo kwa wengine. Sote tunafaa kuungana katika kuangamiza ufisadi kwani uovu huu haufai. Tunafaa kuziba ufa ili tusijenge ukuta.

- |  |  |
|--|--|
| <p>41. Kulingana na aya ya kwanza</p> <ol style="list-style-type: none"> <li>watu hutenda ufisadi hadharani.</li> <li>ufisadi mara nyingi hufanyika kisiri.</li> <li>wanaotenda ufisadi</li> <li>watu wote ni wafisadi.</li> </ol> <p>42. Madhara ya ufisadi ni kuwa,</p> <ol style="list-style-type: none"> <li>huwafanya watu kutajirika.</li> <li>unatekelezwa na watu wachache.</li> <li>huangamiza maisha ya watu wanaoundeleza.</li> <li>huathiri maisha ya watu katika jamii na nchi.</li> </ol> <p>43. Mienendo inayokiuka sheria ni ile ambayo,</p> <ol style="list-style-type: none"> <li>hairuhusiwi kisheria.</li> <li>inaambatana na sheria.</li> <li>haijawekwa katika sheria.</li> <li>inaendelezwa na wachache.</li> </ol> <p>44. Katika nchi za Kiafrika, maskini</p> <ol style="list-style-type: none"> <li>wameanza kutajirika.</li> <li>wanakuwa maskini zaidi.</li> <li>ndio wanaoendesha ufisadi.</li> <li>na tajiri wamekuwa sawa.</li> </ol> <p>45. Viongozi huendeleza vipi ufisadi?</p> <ol style="list-style-type: none"> <li>Wanatumia pesa za umma kwa miradi ya maendeleo.</li> <li>Wazingatie haki wanapotoa hukumu.</li> <li>Wanatumia mali ya umma kwa manufaa yao binafsi.</li> <li>Wanashirikiana na wananchi kuendeleza sehemu zao.</li> </ol> | <p>46. Mahakimu wanapokea hongo ili,</p> <ol style="list-style-type: none"> <li>waamue kesi kwa mapendeleo.</li> <li>wazingatie haki wanapotoa hukumu.</li> <li>wayaruhusu magari yasiyo na vidhibiti mwendo.</li> <li>wawafunge jela wahalifu wakikamatwa.</li> </ol> <p>47. Wahalifu wakiachiliwa huru,</p> <ol style="list-style-type: none"> <li>wataangamizwa na wanajamii wengine.</li> <li>uhalifu utapungua katika jamii.</li> <li>mahakimu watakosa kazi katika nchi.</li> <li>maovu yataendelea katika jamii.</li> </ol> <p>48. Si kweli kusema kuwa,</p> <ol style="list-style-type: none"> <li>polisi wamelaumiwa kwa kushiriki ufisadi.</li> <li>ufisadi unaungwa mkono na wote.</li> <li>madhara ya ufisadi yanaiathiri jamii.</li> <li>ufisadi unajitokeza kwa njia mbalimbali.</li> </ol> <p>49. Watu waovu wakiadhibiwa katika jamii,</p> <ol style="list-style-type: none"> <li>watu wataona madhara ya uovu wajiepushe nao.</li> <li>utoaji hongo hautapungua katika jamii.</li> <li>mahakimu na polisi wengi wataacha kazi.</li> <li>wengi watashiriki ufisadi ili kuepuka adhabu.</li> </ol> <p>50. Wito wa mwandishi wa makala ni kuwa,</p> <ol style="list-style-type: none"> <li>polisi na mahakimu waachishwa kazi ili kuangamiza ufisadi.</li> <li>tushirikiane ili kuyatetea matendo ya ufisadi.</li> <li>kila mmoja awajibike ili kumaliza ufisadi.</li> <li>tutafute kuta zenye nyuta na kuzirekebisha kote.</li> </ol> |
|--|--|